



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

TANGAZO TANGAZO TANGAZO

MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA YA NGARA ANAWATANGAZIA WAFANYABIASHARA WOTE AMEPOKEA MWALIKO KWA WAFANYABIASHARA KUSHIRIKI MAANDALIZI YA MAONYESHO YA 24 YA WAJASIRIAMALI WADOGO WA KATI WA JUMUIYA YA AFRIKA YA MASHARIKI ALIMAARUFU KAMA NGUVU KAZI/JUA KALI YANAYO FANYIKA KWA MZUNGUUKO KATIKA NCHI WANACHAMA WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI KWA MWAKA HUU YANATAZAMIWA KUFANYIKA NCHINI SUDAN YA KUSINI KATIKA JIJI LA JUBA TAREHE 26 OKTOBA MPAKA 06 NOVEMBA 2024.

MADHUMUNI YA MAONYESHO HAYA AMBAYO NI YA 24 TOKA KUENZISHWA KWAKE NI KUWEZESHA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI WANAJOJHUSISHA NA SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZISIZO RASMI KURASIMISHA SHUGHULI ZAO KWA KUWAPATIA FURSA ZA KUTANGAZA BIDHAA ZAO, KUBADILISHANA TAARIFA, KUKUZA UJUZI NA KUKUZA MASOKO YA BIDHAA NA HUDUMA.

KWA FURSA HII ANAWAKARIBISHA KUCHANGAMKIA NAFASI HII ADHIMU KIUCHUMI KWA KUKUTANA NA AFISA VIWANDA BIASHARA NA UWEKEZAJI KWA AJILI YA UFAFANUZI NA UJAZAJI WA FOMU YA USAJILI KWA WATAKAO KUWA TAYARI KUSHIRIKI.

IKUMBUKWE KUWA HII NI FURSA KUBWA YA KUFUNGUA
ZAIDI MIPAKA YETU KIBIASHARA KUCHOCHA UKUAJI
KIPATO NA UKUAJI WA AJIRA.

TUHIMIZANE ILI KUWEZA KUSHIRIKI KWA WINGI TUKIWA NA
BIDHAA ZETU, BUSINESS CARDS, MAANDIKO MBALIMBALI
YA HUDUMA NA KUTANGAZA VIVUTIO TULIVYO NAVYO
KATIKA TAIFA NA WILAYA YETU.

WATAKAOKUWA TAYARI KUSHIRIKI WATAFANYIWA
SEMINA MAALUMU YA KUWAANDAA KWA AJILI YA
MAONYESHO HAYO. MIMI NITASHIRIKI WEWE JE?

NI WAKATI WA KUJITANGAZA NA KUFANYABIASHARA
ASANTENI NA KARIBUNI SANA


Emmanuel P. Kulwa

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NGARA

S.L.P 30, Ngara, Simu:028 2226016, Nukushi:028 2226152, Barua pepe:ded@ngaradc.go.tz,
Tovuti: www.ngaradc.go.tz